

# Hatua za dhana ya SHEP

## Hatua 1: Kushirikisha malengo na wakulima

Warsha ya kutambulisha mbinu ya SHEP kwa wakulima.

## Hatua 2: Wakulima kutambua hali na soko

Kutunza kumbukumbu za mapato ya shamba na utafiti wa awali hufanywa na wakulima.

← Kuunganishwa na wasambazaji wa pembejeo.

## Hatua 3: Wakulima kufanya maamuzi

Wakulima kuamua zao la kuzalisha na kutengeneza kalenda ya zao kwa kuzingatia utafiti wa soko.

## Hatua 4: Wakulima kujiandaa na ufumbuzi

Maafisa wa wilaya na maafisa ugani kutoa mafunzo ya kitaalamu kwa wakulima.

# Simulizi za mafanikio

Kikundi cha **Maisha Bora** cha Bumbuli kilikusanya taarifa za bei kutoka masoko mbalimbali ya Tanga na Dar es salaam, kisha kikapata faida ya Tsh milioni 4.4 kutokana na kulima nyanya ekari 1, iliyowasaidia kukuza uzalishaji wa mbogamboga, kutengeneza pikipiki, au kuanza biashara mpya, mf. kioski.



Kikundi cha **Nguvukazi group** cha Moshi kilitengeneza mtandao wa biashara na taasisi mbalimbali mf. Benki ya NMB ili kupata mkopo na Seed Co. ili kuanzisha mashamba darasa. Walipata milioni 9.5 kwa kutumia SHEP Pamoja na Utafiti wa soko. Pia walipata mkopo wa 4-4-2 wa halmashauri na kutengeneza kitaru nyumba chenye mfumo wa umwagiliaji wa matone kinachowawezesha urahisi mkubwa kubadilisha muundo wao wa uzalishaji ili kutana na mahitaji ya soko.



Imetolewa Agosti 2022

# TANSHEP

Wizara ya Kilimo na shirika la maendeleo la Japan (JICA) wamekuwa wakihamasisha **mbinu ya SHEP** kwa maendeleo ya kilimo cha bustani Tanzania

## SHEP ni nini ?

- **SHEP** ni kifupi cha **S**mall-scale **H**orticulture **E**mpowerment & **P**romotion.
- Ni mbinu ya ugani iliyobuniwa na JICA Kenya na sasa inatekelezwa katika nchi 23 za Afrika ikiwemo Tanzania.
- Tanzania kuna kauli mbiu ya SHEP isemayo, **"Anzia Sokoni, Malizia Shambani, Kwa Kipato Zaidi."**
- Kama kauli mbiu isemavyo, SHEP huanza na wakulima kufanya "Utafiti wa Soko" kisha huimarisha ulimaji kulingana na mahitaji ya soko, ili kubadilisha kilimo kutoka **"kulima na kuuza"** kwenda **"kulima kwa ajili ya kuuza"**



Kwa taarifa zaidi tafadhari tuma barua pepe kwenda: [tanshep.kilimo@gmail.com](mailto:tanshep.kilimo@gmail.com)





# Namna ya kufanya utafiti wa soko.

## Ubunifu wa mkulima kwenye utafiti wa soko ni muhimu!

Utafiti wa soko wa SHEP ni **"mkulima kwanza"**. Unapaswa kufanywa na wakulima wenyewe. Kabla ya utafiti wakulima wanapaswa kuchagua mazao ya kufanyia utafiti, mf. mazao walio na uzoefu nayo na yale mapya, ili utafiti uende kiurahisi.

## Fanya Utafiti wa soko kabla kuanza Uzalishaji.

Kwa ufahamu wa mahitaji ya soko, wakulima wanaweza kufanya mpango mkakati wa uzalishaji Pamoja na kuchagua mazao/aina ya mazao, ubora unao kusudiwa/muda wa kuvuna n.k ili kupata faida kubwa.

## Kazi ya Maafisa wa halmashauri na maafisa ugani

Kusaidia wakulima kupanga utafiti wa soko na kupanga masoko halisi yanayolengwa ambayo yanaweza kutembelewa mara kwa mara. Kuweka miadi na meneja wa masoko na kumuomba utambulisho wa wakulima kwa wanunuzi wakubwa.

## Endelea kufanya Utafiti wa Soko mara kwa mara !!

Kuendelea kufanya mawasiliano na wanunuzi husaidia kutambua mabadiliko ya mahitaji sokoni na kutafuta masoko mazuri.

### Mfano wa Maswali ya Utafiti wa Soko

Ni mwezi upi bei inakua juu?

Hotel yako inahitaji mboga gani za majani?

Tafadhali niambie ubora wa maboga lishe unaoutaka.

Ni ukubwa gani na rangi gani inayopendelewa?

Ni mwezi upi bei inakua chini?

Tutaleta mazao hapa au utayafuata shambani kwetu?

